**TAARIFA YA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA SERIKALIMTANDAO (e-GA) MHA. BENEDICT NDOMBA, KWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YARAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE.GEORGE SIMBACHAWENE (MB), KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA NNE (4) CHA MWAKA CHA SERIKALI MTANDAO**

**FEBRUARI 6, 2024 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.**

---

***Mhe. George Simbachawene (Mb);*** *Waziri wa Nchi, Ofisi yaRais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

***Mhe. Dadi Horace Kolimba****; Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha,*

***Ndug; Juma Mkomi****; Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma,*

***Dkt. Jasmine Tiisekwa;*** *Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Bw. Yusuf Hamad Rashid;*** *Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ),*

***Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,***

***Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali,***

***Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao,***

***Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana;***

***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kutuwezesha kukutana hapa leo katika Kikao Kazi hiki cha nne (4) cha mwaka cha Serikali Mtandao.

Kipekee nikushukuru **Mhe. Waziri,** kwa kukubali na kuitikia wito wetu wa kushiriki nasi hapa leo. Natambua kuwa, unayo majukumu mengine muhimu ya kitaifa, lakini umeweza kutenga muda ili ushiriki nasi katika kikao kazi hiki muhimu cha Serikali Mtandao. Uwepo wako hapa unatokana na dhamira ya dhati uliyonayo, ya kuhakikisha jitihada za Serikali Mtandao nchini zinaimarika kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na usimamizi madhubuti wa Ofisi yako. Tunakushukuru na kukukaribisha sana katika Kikao kazi hiki.

Nitoe shukrani zangu za dhati kwa Viongozi na Watumishi wote wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma, sekta Binafsi na Waandishi wa Habari kwa kushiriki nasi katika Kikao Kazi hiki. Uwepo wenu hapa leo, unaonyesha dhamira yetu ya pamoja katika kuleta mageuzi na kuboresha utendaji wa Serikali Kidijitali na utoaji wa huduma kwa umma.

**Mhe. Waziri;**

Mamlaka ya Serikali Mtandao(e-GA), ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019, ikiwa na majukumu ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao katika taasisi za

umma, pamoja na kusimamia uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma.

Dira ya Mamlaka ni kutambuliwa kuwa Taasisi inayoongoza kwa ubunifu katika kuwezesha matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma kwa umma. Dira hii imekuwa nguzo kwa Mamlaka, katika kuhakikisha inatekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia matumizi ya TEHAMA Serikalini, ili kurahisisha utendaji kazi ndani ya Serikali na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma.

Aidha, Mamlaka imeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na; Kuzijengea Uwezo Taasisi za Umma Kutekeleza Jitihada za Serikali Mtandao kwa kutoa mafunzo mbalimbali ya Serikali Mtandao, Kushirikiana na Wadau wa Utekelezaji wa Serikali Mtandao ikiwemo Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar ili kuhakikisha Serikali Mtandao inaimarika kote Tanzania bara na Visiwani, Kutoa ushauri na msaada wa kiufundi kwa Taasisi za Umma, Kukagua, Kupitia, Kutathmini na Kushauri kuhusu hali ya Usalama wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA pamoja na Kujenga mifumo na miundombinu shirikishi na ya Kisekta ya TEHAMA katika taasisi za umma.

Ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka unatokana na usimamizi mahiri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nitumie nafasi hii kukushukuru **Mhe. Waziri** pamoja na viongozi wengine wa Wizara, kwa usimamizi mzuri wa kuhakikisha e-GA inasimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao, ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA Serikalini yanazingatiwa na kuongeza tija na ufanisi katika utendaji wa serikali na katika kuwahudumia wananchi.

**Mhe. Waziri,**

Kama tunavyofahamu, **Rais wa Jumhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** amedhamiria kuwa na Serikali ya Kidijitali, kwa kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma ili kufikia malengo ya kuwa na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii katika taifa letu. Dhamira ya Mhe. Rais imekuwa ya wazi na dhati kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara yako imekuwa ikitenga fedha za kutosha katika miradi mbalimbali ya TEHAMA. Kwa niaba ya Mamlaka ya Serikali Mtandao tunaomba umfikishie salamu na shukrani zetu **Mhe. Rais.**

Katika kuhakikisha kuwa dhamira yake ya kuwa na Serikali ya Kidijitali inafikiwa, **Mhe. Rais** ameelekeza tuhakikishe kuwa Mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma inaunganishwa na kubadilishana taarifa. Maelekezo haya ya **Mhe. Rais,** yanaenda sambamba matakwa ya Kifungu cha 48(2) cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019.

Katika kutekeleza maelekezo haya, Mamlaka imefanikiwa kujenga mfumo unaowezesha mifumo ya TEHAMA ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa, ujulikanao kama ***Government Enterprises Service Bus*** **(GoVESB),** ambapo hadi sasa **taasisi za umma 109** zimeunganishwa na **mifumo 117** imesajiliwa. Hii ni moja kati ya jitihada nyingi za Serikali Mtandao zilizotekelezwa na kusimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za umma, ambazo zinahusisha matumizi ya miundombinu na mifumo mbalimbali ya TEHAMA shirikishi na ya kisekta katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

**Mhe. Waziri,**

Kikao hiki cha siku tatu (3), ambacho unakifungua hapa leo, kinawakutanisha takriban wadau 1,000 wa Serikali Mtandao, kutoka katika taasisi na mashirika mbalimbali ya umma wakiwemo; Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Makatibu Tawala Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Vitengo na Idara za TEHAMA, Maafisa TEHAMA pamoja na watumiaji wengine wa TEHAMA katika taasisi hizo kwa lengo la kujadili na kutoa taarifa ya hali ya utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao katika taasisi za umma, kwa maana ya mafanikio yaliyopatikana hadi sasa na changamoto zake, pamoja na kuazimia hatua za kuchukuwa ili kukabiliana na changamoto hizi, tuweze kufikia dhamira ya kuwa na Serikali ya Kidijitali.

Hivyo, kwa muda wa siku tatu za kikao kazi hiki mada mablimbali zinazohusu utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao zitawasilishwa na wataalamu wa TEHAMA, kutoka katika taasisi mbalimbali za umma. Washiriki watajadiliana kuhusu mbinu bora zaidi za kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao kutokana na maendeleo ya sasa ya teknolojia, ikiwemo kuainisha changamoto na namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Vilevile, itatolewa taarifa ya utekelezaji wa maazimio 12 yaliyotolewa katika kikao kazi cha tatu cha Serikali Mtandao kilichofanyika mwezi Februari mwaka jana (2023) katika ukumbi huu.

**Mhe. Waziri,**

Kikao kazi hiki kinaongozwa na kaulimbiu isemayo ***“Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa ubadilishanaji***

***salama wa Taarifa" (Compliance to e-Government Policies, Laws, Standards and Guidelines for Secure Electronic Data Exchange)***".

Umuhimu wa kaulimbiu hii ni kusisitiza na kuzikumbusha Taasisi za Umma kuzingatia Sheria, Kanuni, Viwango na mIongozo ya Serikali Mtandao wakati wa kununua au kujenga miundombinu au mifumo ya TEHAMA katika taasisi zao. Lengo ni kuhakikisha miradi na mifumo ya TEHAMA inazingatia matakwa yote yaliyowekwa kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao, ambayo sio tu itasaidia kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma, pia itahakikisha usalama wa taarifa za Serikali, hasa wakati taasisi zinapo badilisha taarifa kupitia mifumo na miundombinu ya Serikali.

**Mhe. Waziri,**

Sambamba na kusimamia ujenzi na uendeshaji wa miundombinu na mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma, Mamlaka pia inakagua, kupitia na kupitisha miradi na miundombinu ya TEHAMA ya taasisi za umma, ili kuhakikisha inazingatia sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo iliyoidhinishwa kwa ajili ya kuhakikisha hakuna urudufu wa jitihada, pamoja na kuhakikisha usalama wa taarifa. Taarifa zitakazotolewa kwenye kikao hiki, zitaainisha matokeo ya kazi zilizofanywa katika kutelekeza jukumu hili na hatua zilizochukuliwa, yaani kupitisha na kusitisha miradi na mifumo ya TEHAMA ya taasisi mbalimbali za umma.

**Mhe. Waziri,**

Mafanikio ya kikao hiki yanatokana na ushirikiano mkubwa tulioupata kutoka katika Ofisi yako, pamoja na wadhamini mbalimbali. Kwa ruhusa yako naomba kuwatambua wadhamini wote wa Kikao Kazi hiki cha Nne cha Serikali Mtandao.

**Mhe. Waziri;**

Baada ya kusema hayo, naomba sasa nimkaribishe Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao **Dkt. Jasmine Tiisekwa** ili aweze kutoa salamu.

Asanteni sana kwa kunisikiliza,

***"Karibu tuijenge Serikali Kidijitali"***